


RIPOTI UZUIAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI KWA WASICHANA NA WANAWAKE WACHANGA



NCHINI KENYA

MAELEZO KUHUSU NCHI:

Idadi ya watu (makisio ya mwaka 2006):	34,707,817 ¹
Matazamio ya muda wa kuishi (mwaka 2006):	wanaume – miaka 51; wanawake – miaka 50 ²
Asilimia ya watu walio chini ya kipimo cha umaskini cha dola 1 (\$1) kwa siku:	46% ³
Asilimia ya watu walio chini ya umri wa miaka 15:	42.1% ⁴
Kiasi cha wanawake wanaojuwa kusoma na kuandika ikilinganishwa na kile cha wanaume (umri wa miaka 15–24) ⁵ (mwaka 2004):	hakuna data
Umri wa wastani wa wanawake kuolewa mara ya kwanza (miaka 25–29)	miaka 20 ⁶
Umri wa wastani wa wanaume kuolewa mara ya kwanza (umri wa miaka 15–49):	hakuna data
Umri wa wastani wa wanawake kufanya mapenzi mara ya kwanza (umri 15–49) ⁷ :	hakuna data
Umri wa wastani wa wanaume kufanya mapenzi mara ya kwanza (umri 15–49) ⁸ :	hakuna data
Kiwango cha matumizi kwa afya kwa kila mtu (intl \$ mwaka 2004):	Dola 86 ⁹
Idadi ya manesi kwa kila watu 1000 (mwaka 2004)	1:47 ¹⁰
Asilimia ya wanawake wanatotumia njia za upanganji uzazi wenye umri katy 15–49 (1996–2004) ¹¹ :	39% ¹²
Kiwango cha uzazi (makisio ya 2000–2005):	watoto 5 kila mama ¹³
Kiwango cha vifo vya kina mama wanapoijifungua kwa kila watoto 100,000 (1990–2004):	410 ¹⁰
Makabila:	Kenya ina makabila 42, wengi wake wakiishi mashambani ¹⁴
Dini:	Waprotestanti 43% Wakatoliki 33% Waislamu 10% Imani za kienyeji 10% nyingine 2% ¹⁵
Luga:	Kiingereza (luga rasmi) Kiswahili (rasmi) lugha za kienyeji kadha ¹⁶

MAELEZO KUHUSU UKIMWI:

Kiwango cha ueneaji wa ukimwi (umri 15–49)	6.1 (5.2–7.0)% ¹⁴
Idadi ya wanawake (miaka 15 juu) walio na ukimwi (2006):	740,000 (640,000–840,000) ¹⁵
Idadi ya watoto (umri 0–14) walio na ukimwi:	150,000 (55,000–290,000) ¹⁶
Kiwango cha ueneaji wa ukimwi kwa wanawake wachanga (umri 15–24):	5.2% ¹⁷
Kiwango cha ueneaji wa ukimwi kwa wanaume wachanga (umri 15–24):	1% ¹⁸
Kiwango cha ueneaji wa ukimwi mionganoni mwa makabila wa mijini (2000):	27% ¹⁹
Idadi ya vifo vinavyotokana na ukimwi (2006):	140,000 (110,000–170,000) ²⁰
Makisio ya idadi ya mayatima (umri 0–17) kutokana na ukimwi (2005):	100,000 ²¹

MAELEZO KUHUSU KINGA DHIDI YA UKIMWI KWA WASICHANA NA WANAWAKE WACHANGA:

Kutokana na ongezeko la huduma zinazohusiana na ukimwi, kiwango cha ueneaji wa ukimwi kimeshuka katika miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo, wanawake wachanga na wasichana nchini Kenya wangali hatarini ya kuambukizwa ukimwi kutokana na ukoseli wa usawa wa kijinsia na ukoseli wa nafasi za kujideleza kiuichumi kwa wanawake hawa wachanga na wasichana. Kwa mfano, 11.4% ya wanawake wachanga wa umri 15–19 walitumia kondomu mara ya mwisho kufanya mapenzi,²² na uchunguzi wa kimataifa wa huduma za idadi ya watu ulipata kuwa 25% ya wanaume wa umri zaidi ya miaka 30 walikoriki kuwa na mapenzi nje ya ndoa, walikuwa na mapenzi aliyekuwa mdogo kwa miaka 10 kuwalikizo. Wanawake hawa wachanga katika mahusiano haya ya kimpenzi walitaja mapato ya pesa kama sababu kubwa ya kujihusisha katika mapenzi na wanaume waliozwidi umri na uchunguzi huu ukaonyesha kuwa wanawake wachanga hawa hawajali sana kuugua ukimwi – athari ambayo ilitajwa na wachache sana kuwa mojawapo ya athari za kufanya mapenzi nje ya ndoa.²³ Makabaha huwa ndio kundi moja ililo hatarini na kwa sababu ya ukahaba kuwa haramu nchini Kenya, hakuna ushahidi kuhusu kiwango cha maambukizwa pamoa na njia za kuwasaidia. Inakisiva kuwa 17% tya yao wanafikirika na huduma za kinga.²⁴ Mnamo 2001, uchunguzi wenye ncha nyinyi ulihiusha sensa ya makabaha waliozunguma, ulionyesha kuwa ueneenji wa ukimwi mionganoni mwa

UTANGULIZI

RIPOTI HII INANUILIWA KUTOA MUHTASARI WA KINGA DHIDI YA UKIMWI KWA WASICHANA NA WANAWAKE WACHANGA NCHINI KENYA.

Ripoti hii ni moja katika msururu uliotolewa na Muungano wa Kimataifa wa Upangani Uzazi (International Planned Parenthood Federation – IPPF), chini ya Muungano wa Dunia kuhusu Wanawake na Ukimwi (Global Coalition on Women and Aids) na kwa usaidizi wa Hazina ya Watu ya Muungano wa Mataifa (United Nations Population Fund – UNFPA), Waliouqua wakiwa Wachanga (Young Positives).

Ripoti yenye ni kifaa cha utetezi. Inanulia kuongezea na kuboresha harakati za mipango, sera na ufadili zilizochukuliwa kulinga ukimwi mionganoni mwa wasichana na wanawake wachanga nchini Kenya. Walengwa wake wakuu ni wa kitaifa, kiene na kimataifa wanaofanya sera na uamuzi na pia watoaji huduma. Inaendeleza wito wa sera za kilimwengu, kama ziliviyokariiwa katika Azimio la Kisiasa Kuhusu Ukimwi (Political Declaration on HIV/AIDS) kutokana na Mkutano wa Safu ya Juu wa Juni 2, 2006, wa kufuatilia Kikao Maalum Kuhusu Ukimwi cha Baraza la Muungano wa Mataifa (United Nations General Assembly Special Session on AIDS – UNGASS).

Ripoti hii inatoa ufupisho wa hali iliyivo sasa kuhusu njia na huduma za kinga dhidi ya ukimwi kwa wasichana na wanawake wachanga wa umri 15–24, nchini Kenya. Ina uchambuzi wa njia tano kuu zinazosaidia katika kinga dhidi ya ukimwi, nazo ni:


1. Kuwepo Kwa sheria
2. Kuwepo Kwa sera
3. Kuwepo kwa huduma
4. Ufikiaji wa huduma
5. Uhusishaji na haki

Pia inatoa mapendekezo kwa washika dau muhimu ili kuzidisha harakati zinazohusu njia na huduma za kukiinga virusi vya ukimwi kwa wasichana na wanawake wachanga nchini Kenya.

Ripoti hii ni msingi wa utafiti mwingu uliofanywa mwaka 2007 na IPPF, uliohusu utafiti wa ndani kwa kutumia data na ripoti zilizochapishwa, na pia utafiti wa kwenda nje kwa watu nchini Kenya ili kutoa habari halisi. Utafiti huu umeleezewa kwa mapana katika “Ripoti ya Uchunguzi kuhusu Kinga dhidi ya Ukimwi kwa Wasichana na Wanawake Wachanga nchini Kenya” (Research Dossier on HIV Prevention for Girls and Young Women in Kenya) inayoweza kupatikana kwa idhini ya IPPF.

makabaha ulikuwa wa kiwango cha juu kuliko mionganoni mwa wanawake wengine – 75% ikilinganishwa na 30%. Ni nusu tu ya makabaha hawa waliosema kuwa walikuwa wametumia kondomu na wateja wao.²⁵ Zaidi ya haya, kuna tafiti kati ya upangaji na utekelezaji wa huduma zinazohusu masuala ya wanawake, data ikiwa haiinganji na jinsia.²⁶ Hivyo, pana haja ya mifumo ya sera na sheria ili kutekeleza haja na haki za wasichana na wanawake wachanga ili kundi hili liweze kuwa na uhuru kuhusiana na afya ya uke na uzazi, ikiwemo kinga dhidi ya ukimwi, tiba, utunzi na usaidizi.

Hata hivyo, kuna ishara wazi za kufaulu na hivi karibuni kumekuwa na hatua mwafaka zilizochukuliwa. Kwa mfano, Kenya sasa ina mfumo mzuri wa ufuatilaji na utathminni ili kuongoza namna ya kuchukua, kuchunguza, kutumia na kuceana habari ambazo huwezesha kufuata maendeleo yaliyofanywa dhidi ya ukimwi na kusaidia kufanya maamuzi.²⁷ Mpango kabambe wa kuanzisha sera ya kitaifa kuhusu jinsia na maendeleo unaundwa sasa. Vijana na wanawake sasa wamewakilishwa vyema na wanahusiano zaidi katika baraza za uamuzi kama vile National Aids Control Council na Kenya National HIV/AIDS Strategic Plan (KNASP). Ili kuwezesha mabadiliko ya kudumu, jitithada kama hizi zinafaa kuongezewa ili ziwe sehemu ya mpango wa jumla wa kinga ambao umeundwa na kutekelezwa. Ni muhimu kuwa matamshi yaye witemdo kwa wanawake wachanga na wasichana ambaa wamelemewa sana na ukimwi nchini Kenya.



HOJA MUHIMU:

- **Umri halali** wa kuo a kwa wanaume na **kuolewa** kwa wanawake **ni miaka 18.**²⁹
- Umri halali wa mtu kwenda **kwa upimaji ukimwi au kwa huduma yoyote ya afya ya uke na uzazi** bila idhini ya mzazi ni **miaka 18**, kama ilivyo kwa hatua zozote zile za kimatibabu. Hata hivyo, haya hayahusu vijana walioolewa au walio wazito. Mshauri anaweza kutumia hiari yake kwa vijana wa umri wa miaka 15 hadi 18. Vijana walio chini ya miaka 14 wanaweza tu kupata ushauri.³⁰
- **Utoaji mimba** ni halali tu pale **mimba ingehatarisha maisha ya mama au ili kudumisha afya yake kimwili na kiakili**. Utoaji mimba **huu lazima ufanyiwe hospitalini** na daktari aliye na kibali kwa idhini ya mama mwenyewe na bwanake. Maoni ya daktari wa kiakili na daktari wa mwili yanahitajika kabla ya utoaji mimba kufanywa.
- **Sio lazima mtu kupimwa kwa virusi vya ukimwi.** Hata hivyo, makanisa mengi yanapendekezea wachumba kwenda kupimwa kabla ya kufunga ndoa. Kwa sababu hii waumini wengi wamegawanyika kuhusu kwamba hii itaweza kupunguza kuenea kwa ukimwi au la au itaendeleza tu unyanyapaa.³²
- **Mswada wa hatia za kijinsia wa 2006 (The Sexual Offences Act 2006)** una:
 - Hatia 14 jipya, ikiwemo ubakaji na wengi, uambukizaji maksudi wa ukimwi, ulaguzi kwa ajili kutumia kimpenzi na ponografia kutumia watoto.
 - Kutoa vifungo kwa hatia.
 - Kuanzisha kituo cha kuchunguza data za DNA pamoja na usajili wa watoto wanaodhulimiwa kimpenzi.
 - Kule kuchukua kama hatia bugudhi za kimpenzi kwa wanawake.³³
- **Ukahaba nchini Kenya** ni haramu na unashutumiwa. Sheria **inapiga marufuku uuza ji wa mapenzi lakini haiadhibu mteja kwa kuyanunua.** Kwa hivyo, wanawake wanaojihusisha na ukahaba ni **wahalifu** kwa kufanya jambo haramu.³⁴
- Kuwa na sindano na sirinji zilizotumika kunawenza kumfanya mtu ahukumiwe. Hili limewafanya wengi **wanotumia mihadarati ya kujidunga** (IDUs) kutobeba vifaa vya kujidunga. Kwa hivyo watumizi hawa (IDUs) **wanakosa kununua sindano na sirinji** mahali ambapo madawa haya yanatumiwa. Mambo haya yanazua fursa hatari sana za kuambukiza.³⁵
- **Mswada wa kinga na uzuiaji virusi vya ukimwi** nchini Kenya ulipitishwa bungeni mnano Disemba 2006, ijapokuwa **haujasisitizwa vya kutosha bado**. Mswada huu **unatoa haki za watu walio na virusi na unanuilia kupunguza athari za janga hili kwa wananchi.**³⁶
- **Ubaguzi** umezingatiwa katika mswada huu, hasa ubaguzi katika makazi, katika taasisi zote za elimu na kupiga marufuku namna zote za ubaguzi wa watu walio, au **wanakisiwa kuwa na virusi**. Hata hivyo mswada huu hautaji **kinaganaga walio hatarini mno.**³⁷

DONDODA NA MASUALA:

- “Kuna visa ambapo wasichana wadogo **wameishia kutumia namna mbovu sana za kutoa mimba** Kama vile **kutumia vipimo** ya kupindukia vya madawa ya malaria au **madawa makali ya miti shamba** ili kuua vijusi. Jambo hili limesababisha vifo vingi.” (Mazungumzo na makundi lengwa ya wanawake wachanga na wasichana, mashambani, umri 15–26)
- “**Vijana chini ya miaka 18 wanafaa kupata idhini ya wazazi ili kutumia huduma za vituo vya ushauri na upimaji (VCT).** Hii inamaanisha kuwa, vijana wanaojihushisha mno na mapenzi hawatumii huduma hizi.” (Mazungumzo na Makundi – lengwa ya wanawake wachanga na wasichana, mashambani, umri 15–26)
- “Dini na utamaduni huathiri utekelezaji wa sheria. Katika upande **mmoja vipindi hutufunza kuwa tutumie kondomo ikiwa tutafanya** mapenzi, lakini katika upande mwingine dini **hairuhusu kutumia mipira mionganii mwa vijana kwani inawataka wasijihuise kamwe. Kujizuwa ni vigumu.**” (Mazungumzo na Makundi – lengwa ya wanawake wachanga na wavulana, mjini, umri 15–24)
- “**Mswada mpya unaharamisha uambukizaji maksudi wa ukimwi lakini** kwa jumla sana. Hautaji kinaganaga wasichana wadogo na wanawake wachanga.” (Majadiliano Mshauri wa utekelezaji wa Huduma, Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali kuhusu Afya ya Jinsia na Uzazi)
- “Kwa maoni yangu **sheria kuhusu Ukimwi nchini Kenya ni ya jumla sana** na haizingatii kila kundi-husika kivyake” (Majadiliano – Meneja wa Mradi Shirika lisilo la Kiserikali la Kenya)
- “**Sheria za Waislamu zinaruhusu wanawake kuolewa wakiwa na umri wa miaka 15,** bora msichana awe hajalazimishwa kuolewa. Huu ndio umri wa chini kabisa ambapo mwanamke anaweza kuolewa kulingana na sheria za Waislamu.” (Majadiliano – Shehe, Mratibu wa Afya ya Uzazi ya Vijana na Mradi wa Kinga Dhidi ya Ukimwi kwa vijana)
- “Kuwa na **mswada kuhusu ukimwi ni hatua mwafaka sana**, lakini hakuna njia ya kuingilia miktadha ambapo sheria hizi zinaweza kutekelezwa. Kwa mfano, miktadha tofauti ya kitamaduni inayowahatarisha watu mbalimbali katika jamii. Sheria zinaweza kuwepo, lakini **ikiwa sheria haziwezi kupewa nguvu, basi inakuwa muhalii.**” (Majadiliano – Mshauri wa Maendeleo ya Taasisi – UN Agency)
- “**Sheria kwa namna fulani imechangia kuongezea hatari ya kutumia nguvu na kuambukizwa ukimwi kwa wanawake.** Kwa mfano, pale **inakuwa** hatia kwa makahaba **kutafuta riziki kuptitia ukahaba.** Wanasumbuliwa mara kwa mara na askari kwa ajili hii.” (Majadiliano – Afisa wa Mradi, Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali Kuhusu Upangaji Uzazi)
- “Sheria zinaweza kuweka kama vile **Sheria Kuhusu Ukimwi** iliyowekwa mapema mwaka huu. Lakini utekelezaji wa sheria **kama hizi ni changa moto kubwa sana nchini Kenya.**” (Majadiliano – Afisa wa Mradi wa Afya ya Uzazi ya Vijana, UN Agency)



HOJA MUHIMU:

- Lengo la KNASP (2005/6–2009/10) ni kupunguza kuenea kwa ukimwi, kuboresha hali ya maisha ya wale walioambukizwa na walioathiriwa, na kupunguza athari za kiuchumi za janga hili.³⁸ Matakwa muhimu ya KNASP ni:
 - Kuwa na njia inayohusisha sekta nyingi**, ikiwemo kuanzisha mahusiano muhimu na kudhibiti ukimwi katika sekta zote muhimu.
 - Kulenga makundi yaliyo hatarini**.
 - Kulenga jinsia na vijana**.
 - Kushirikisha kikamilifu watu waliouguwa ukimwi katika utekelezaji wa njia hii**.
 - Usaidizi uliokitwa katika ushahidi.
 - Njia ya ushirikishi na kutia nguvu**.
 - Kusaidia harakati zinazofanywa kieneo na kimataifa.³⁹
- KNASP 2005/6–2009/10 inasisitiza **kusaidia watu waliouguwa ukimwi**. Katika **mwaka 2006**, nia ilikuwa ya kuwapa watu 240,000 madawa ya kupunguza athari za virusi (ARVs), ijapokuwa ni watu 120,026 tu waliofikiwa.
- Mbinu KNASP 2005/6–2009/10 zinazotumia kukinga uambukizaji wa ukimwi mionganoni mwa vijana ni kama:
 - Ujumbe kuhusu kinga uliotayarishwa na kuwasilishwa** vizuri. Vijana wengi wamesikia kuhusu virusi na ukimwi lakini ni 53% tu ya wanawake wachanga na 60% tu ya wanaume wachanga wanaojua kuwa kondomu hupunguza hatari ya kuambukiza ukimwi.
 - Habari zinazovutia vijana** kuhusu ukimwi na afya ya uzazi pamoja na huduma nyiningezo.
 - Kuzindua mfumo wa elimu ili kutoa **mpango mwafaka kuhusu kinga na utunzaji vijana katika shule**.
 - Kuboresha uwezo wa wasichana kupata elimu na ufundi** na kuhakikisha **haki zao**.
 - Kujenga uhusiano na mashirika ya vijana**.⁴⁰
- KNASP 2005–2009 inanua kuzidisha kutangaza hatari **kwa wale walio katika hatari ya kuambukizwa ukimwi** pamoja na athari zake katika taifa. Hii inamaanisha kuwa makundi yafuatayo yatalengwa:
 - Mke na mume amba moja ndiye aliyeambukizwa**.
 - Makahaba**.
 - Mayatima na watoto walio hatarini**.
- KNASP 2005–2009 inalenga kuungeza huduma za kukinga uambukizaji wa mama kwa mtoto nchini kwa **kuungeza idadi ya akina mama wajawazito wanaopewa madawa ya kupunguza athari za ukimwi (ARVs)** ili **kiwango cha watoto wanaozalivu na virusi** vya ukimwi ipungue toka 33% hadi chini ya 23%.⁴² Pia kuna **miongozo kuhusu uzuiji wa maambukizo ya mama kwa mtoto inayoeleza utunzaji** wa wanawake wajawazito na wanaougua ukimwi katika sehemu zote.⁴³
- Huduma ya ushauri na upimaji (VCT)** ni bure katika taasisi zote za umma⁴⁴ kuna Miongozo ya Kitaifa Kuhusu Ushauri huu na **Upimaji (VCT)** iliyochapishwa na wizara ya Afya, na inayotoa maelekezo kuhusu utoaji huduma.⁴⁵ Kuna **mipango ya kuungeza upimaji katika msingi wa kujitoo**.⁴⁶
- Wizara ya afya pia imetoa **miongozo na sera kuhusu tiba na utunzaji wa maambukizo ya zinaa (STIs)**.⁴⁷
- Kijitabu cha Data Kuhusu Ukimwi**, Kenya ina habari kuhusu kuenea kwa ukimwi kutegemea umri na jinsia.⁴⁸
- KNASP inasisitiza **ongezeko katika usambazaji wa kondomu pamoja na habari kuhusu kondomu za wanaume na za wanawake**, na inaweka malengo mahsusini ya:

- Angaa 40% ya wanawake na 65% ya wanaume katika kiwango cha umri wa 15–24 **wawe washatumia kondomu wanaopofanya mapenzi hivi karibuni**.
- 85% ya wanawake na wanaume wa umri wa 15–24 waweze **kutambua vyema njia za kuzuia kuambukizwa ukimwi kupitia ngono**.⁴⁹
- KNASP 2005–2009 inapanga **kuanzisha mbinu mahsus za kutekeleza** uzuijia wa ukimwi na matakwa mengine yahusianayo na ukimwi ya **wanaotumia mihadarati ya kujidunga (IDUs)**, ijapokuwa hajatajwa mbinu hizi mahsusini ni zipi.⁵⁰
- Mamlaka ya **Almashauri ya Kitaifa la Kudhibiti Ukimwi (NACC)** ni kutoa mfumo wa sera na mbinu za **kupanga na kueneza rasilimali ya ukimwi na kutoa utunzaji** na usaidizi kwa wale walioambukizwa na walioathiriwa katika Kenya.⁵¹

DONDODO NA MASUALA:

- "Pengine jina la sua la lingebadilishwa badala ya '**Elimu ya jinsia**' iwe '**Mafundisho ya Mbinu za Maisha**' ili kubabalika mionganoni mwa wazazi na makanisa." (Mazungumzo na Kundi – lengwa la Wanaume Wachanga na Wavulana Mjini umri 15–24)
- "**Iliyo sasa walioambuki-zwa wanadhalalishwa na hivyo basi wanaogopa kujitekeza hadharani**. Watu wanafaa kutiwa moyo ili kujua hali zao na **waishi kwa kujikubali bila kubaguliva**." (Mazungumzo na Kundi – lengwa la wanawake wachanga na wasichana, mijini, umri 15–24)
- "Sera moja muhimu inayohitajika ni sera kuhusu elimu isiyobagua ya jinsia shulen. **Wazazi, wanafaa kuelimishwa kuhusu masuala muhimu yanayohusu** vijana ili waweze kuelewa umuhimu wa elimu ya jinsia katika kupunguza matatizo fulani magumu katika jammii za leo yanayohusu afya ya uzazi na ukimwi." (Majadiliano – Mshauri wa Utekelezaji wa Huduma, Shirika la kimataifa lisilo la Kiserikali, Kuhusu Afya ya Jinsia na Uzazi)
- "**Hakuna elimu rasmi ya jinsia shulen kwa sasa. Kumekuwa na mjadala kuhusu kuanzisha elimu ya jinsia**, lakini kila wakati inapodokezwa, makanisa na wazazi hawajakubaliana." (Majadiliano – Meneja wa Mradi, Shirika la Kenya lisilo la kiserikali Kuhusu Afya ya Jinsia na Uzazi)
- "**Sijasoma kwa mapana na marefu**, lakini ninaamini kuwa kuna **sera nydingi** ni itifaki pamoja na **miongozo iliyonuiliwa kuboresha kinga dhidi ya ukimwi**." (Majadiliano – Shehe, Mratibusi wa Afya ya Uzazi ya Vijana na Mradi wa Kinga dhidi ya Ukimwi kwa Vijana)
- "**Serikali inafaa kufanya maksudi mpango wa kuhakikisha kuwepo kwa njia za kulinga mimba**. Kwa sasa serikali haikadiri katika bajeti ununuza wa kondomu, bali UNAIDS ndio hununua kondomu na kuzisambaza." (Mshauri wa Maendeleo ya Taasisi – UN Agency)
- "**Pana haja ya kupunguza vikwazo vya uratibu serikalini** katika kutekeleza huduma muhimu. Kanuni kuwa lazima vijana wadogo wapate idhini ya mzazi ili kupata huduma za kinga pamoja na sheria kuhusu **utoaji mimba na ukahaba zinafaa kuangaliwa upya ili kuwiana vyema** na hali iliyoko sasa ya wasichana na wanawake wachanga." (Majadiliano – Afisa wa Mradi wa Afya ya Uzazi ya Vijana, UN Agency)
- "**Serikali inafaa kukadiria matumizi na kuanzisha sera zitakazowezesha wasichana na wanawake wadogo amba** hawajajiriwa waweze kupata huduma, sana sana **mashambani ambako malipo japo kidogo, yangali ni kizuiji kwa wanawake**." (Majadiliano – Afisa wa Mradi wa Afya ya Uzazi kwa Vijana; UN Agency)
- "**Ingekuwa bora kama serikali ingeweka mbinu** za kuweza kuondoa tatioo kuu la **unyanyapaa na ubaguzi**." (Mwenyekiti-Shirika la Kitaifa la Watu Waliouguwa Ukimwi – National PLHIV Network)



HOJA MUHIMU:

- Kuna **vituo 4,203** nchini ambako **huduma za afya ya jinsia na uzazi** zinatolewa.⁵²
- **Huduma ya upimaji na tiba ya maambukizo ya zinaa imejumuishwa katika idara ya matibabu ya jumla ya mahospitali** kwa hivyo, kuna huduma chache mahsusisi za maambukizo ya zinaa za kuchunguza na kutibu au hata vituo vya kufanya hivi.⁵³
- Kufikia mwisho wa 2005, kulikuwa na vituo 650 vya ushauri na upimaji (VCT) nchini. **Huduma zote hizi za ushauri na upimaji (VCT) zimeeteuliwa na kuidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya Huduma ya Kukinga Ukimwi/Maambukizo ya Zinaa.** Harakati za kupanua huduma hizi zimeongeza idadi hii hadi vituo **900** nchini **kufikia sasa.**⁵⁴
- Kufikia mwisho **wa 2005**, kulikuwa na **vituo 759** nchini **vya kutoa huduma ya kuzuia uambukizaji ukimwi** wa mama kwa mtoto (PMTCT).⁵⁵
- "Serikali imeanzisha vituo **vya kutunza waliouguwa ambapo watu walio na virusi (PLHIV)** wanaweweza **kupata matibabu**, ushauri **na usaidizi mwingine wa kiakili- kijamii.**⁵⁶
- Kupitia Huduma ya Kitaifa ya Mafundisho ya Afya ya Jamii (FLTP), ilio idara katika wizara ya Afya, **kuna miradi inayojaribu kuboresha mawasiliano na suala la ukimwi pamoja na shida nyingine za kijamii.** Mradi wa Kitaifa wa Kuzuia Ukimwi na Maambukizi ya Zinaa (NASCOP) pia una mipango inayoshughililia mawasiliano kati ya mwanamke na mwanamume.⁵⁷
- Kuna **vituo 20** vya vijana nchini ambayo vinatoa huduma za afya ya jinsia na uzazi kwa vijana.⁵⁸
- Huduma za kijamii za uuzaji zinapanuliwa ili **kuimarisha kuwepo kwa na uwezo wa kununua** kondomu za wanaume, sanasana katika maeneo yaliyo katika hatari zaidi. Huduma hii ambayo kwa sasa imo mikoa 4 itapanuliwa ili kufikia mikoa yote, ikisaidiwa na **Taasisi ya Elimu ya mawasiliano (IEC)** inayolenga makundi yaliyo hatarini. KNASP pia inasaidia kusambaza **kondomu za wanawake** kama njia ya kuwawezesha kufanya mapenzi salama. Lengo kufikia 2010 ni kusambaza kondomu milioni 160 kila mwaka.⁵⁹
- Kuna vituo **5,170** vya **kutoa huduma kwa wanawake wajawazito (ANC)**, ambapo vituo 1,090 vinahusu uzuaij wa maambukizi ya mama kwa mtoto (PMTCT). **Kwa jumla ni vituo 2000.**⁶⁰ Idadi hii inazidi kuongezeka kadri huduma zinavyopanuliwa.⁶¹
- Wanaotumia mihadarati ya kujidunga (IUDs) hawajatambuliwa kama moja wapo wa makundi yaliyo hatarini nchini Kenya na hivyo huduma kwao ni chache. Hata hivyo, kuna mashirika 11 yaliyoorodheshwa kama vituo vya huduma katika mtandao wa Tume ya Kitaifa ya Kupambana na Madawa ya Kulevya, Kenya (NACADA).⁶²

DONDODA NA MASUALA:

- "Huko mashambani, utapata vifaa **vya kutoa kondomu ambavyo havina kondomu.** Vifaa hivi vinabaki vitupu kwa muda mrefu. Vinafaa kuwa mahali ambapo vijana wanaweweza kupata kondomu wanapohitaji, na mara wanapozikosa huendelea kufanya mapenzi bila kuwa nazo." (Mazungumzo na Kundi – lengwa la wanawake wachanga na wasichana, mashambani, umri 15–26)
- "Kuna kampeni na huduma nyingi kuhusu kuzuia ukimwi **lakini matokeo yake hayajaonekana bado.**" (Mazungumzo na Kundi – lengwa la wanaume wachanga na wavulana, mjini, umri 15–24)
- "Utumizi wa picha utaonyesha dhahiri athari za ukimwi kwenye miili ya binadamu na hivyo kuwafanya wale ambao hawajaambukizwa kuwa na tahadhari kubwa." (Mazungumzo na Kundi – lengwa la wanawake wachanga na wasichana, mjini, umri 15–24)
- "Utunzi na msaada kwa wasichana na wanawake wachanga **umekosekana kabisa**, wengine wao wakiwa wamefukuzwa kutoka nyumbani na wazazi wao kwa kuwa na virusi." (Majadiliano – Mshauri wa Utekelezaji Huduma, Shirika la Kimataifa lisilo la kiserikali kuhusu Afya ya Jinsia na Uzazi)
- "Pamekuwa na **maendeleo kabambe katika upanuzi wa huduma za ushauri na upimaji (VCT).** Katika maeneo ambapo hapana vifaa vya kudumu, huduma nyepesi za kuhamahama zinatolewa, lakini **hakuna kliniki zinazolenga hasa wasichana na wanawake wachanga pekee.**" (Majadiliano – Meneja wa Mradi, Shirika la Kenya lisilo la serikali Kuhusu Afya ya Jinsia na Uzazi)
- "Kwa sababu ya ukimwi, **jamii ya Waislamu imeruhusu utumizi wa kondomu ili kuzuia maambukizi.** Utumizi wa kondomu utakubaliwa pale ambapo nia ya maharusi ni kujikinge dhidi ya kuambukizwa ukimwi na kuzuia mamba." (Majadiliano – Shehe, Mratibu wa Kinga dhidi ya Ukimwi kwa vijana)
- "Kuna vibango vingi mijini kuliko mashambani vinavyosambaza habari kuhusu uzuaij wa ukimwi. **Huduma za ushauri na upimaji (VCT) hazitoshi katika mashambani.**" (Majadiliano – Mshauri wa Maendeleo ya Taasisi – UN Agency)
- "Vituo vya ushauri na upimaji (VCT), vya kuzuia maambukizi ya mama kwa mtoto (PMTCT) na vya kutoa madawa ya kupunguza athari za ukimwi (ART) havilengi wasichana na wanawake wachanga. Vipo ndio, lakini havitoshi, sana sana vya ART. Wengi wanaotaka kusaidiwa navyo hawavipati." (Majadiliano – Afisa wa Mradi, Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali kuhusu Mpango wa Jamii)
- "Huduma za ushauri na upimaji (VCT) zilizoko hazivutii vijana. Zinalenga watu wote wazima kwa jumla na havilengi kutoa huduma kwa vijana. **Hii huwa ni kikwazo kwa wasichana na wanawake wachanga katika kupata huduma.**" (Majadiliano – Afisa wa Mradi wa Afya ya Uzazi ya Vijana, UN Agency)
- "Ni hivi majuzi tu ambapo mipango imeanzishwa ya kujaribu kuwasaidia **watumizi wa mihadarati kwa kutoa habari** kuhusu hatari ya kuambukizwa virusi kwa kutumia pamoja sindano na sirini." (Majadiliano – Mwenyeketi, Shirika la Kitaifa la watu waliogua Ukimwi – PLHIV Network)



HOJA MUHIMU:

- Kwa kweli kuna vikwazo kadhaa **vya kijamii, kimipango na kifedha** kwa wasichana na wanawake wachanga katika kupata huduma nchini Kenya ikiwemo:
 - Misimamo hasi ya familia**, wanajamii na wahudumu wa afya.
 - Unyanyapaa** unaohusiana na virusi na ukimwi unawafanya watu waogope kutembelea vituo vya ushauri na upimaji (VCT).
 - Ukosefu wa habari** kuhusu huduma zilizoko.
 - Umbali** wa huduma hizi na gharama ya usafiri, hasa mashambani.
 - Ukosefu wa **faragha na uaminifu** ni kikwazo kingine nchini Kenya.
 - Tamaduni zinazohusu **ubaguzi wa kijinsia**.
Vikwazo vingi hivi huwaathiri hasa wasichana na wanawake wachanga wanaoishi mashambani.⁶³
- Kuna vituo 8 tu** katika hospitali za serikali vinavyotoa huduma inayohusiana na vijana **katika wilaya 71 nchini Kenya**.⁶⁴
- Ushauri wa hiari na upimaji (VCT) unatolewa kwa ye yote apendaye na aliye na umri wa 18** kwenda juu, pamoja na walioolewa kabla ya kutimiza miaka 18, walio wajawazito au makahaba watoto. Washauri hutumia uamuzi wao katika kusaidia vijana hao wadogo wanaotaka ushauri na upimaji. **Kuna tofauti za kijinsia kuhusiana na wanaohitaji huduma za ushauri na upimaji**. Kat i ya mwaka 2001 na 2004, 56% ya wateja walioendea huduma za ushauri na upimaji walikuwa wanaume.⁶⁵
- Vituo vyote vya ushauri na upimaji vilivyoko katika hospitali za umma kwa hivi sasa vinatoa huduma bure,**⁶⁶ japo vinaweza kuanza kulipisha ikiwa vitaidhinishwa na wakala inayosimamia kituo. Hata hivyo, washauri wanawenza kuondoa malipo ikiwa watathibitisha kuwa mteja hawezikulipa.⁶⁷
- Matibabu ya maambukizo ya zinaa (STIs)** kwa kutumia njia ya kutunza dalili yanatolewa bure katika hospitali za serikali.⁶⁸
- Vituoni, **misimamo hasi ya wanaotoa huduma** inaweza kuzuia **wasichana na wanawake wachanga** wanaotafuta habari kutoendeua usaidizi katika vituo hivi.⁶⁹
- Kuanzia Juni 2006, **madawa ya kupunguza athari za virusi (ARVs) yametolewa bure kwa wanaoyahitaji**, wakiwemo wasichana.⁷⁰
- Wanawake wengi, hasa wanaoishi mashambani hawawezi kupata habari** inayohusiana na ukimwi kuitia vyombo vya habari na hivyo basi **hawawezi kupata huduma. Utumizi wa matangazo kuitia vibango** umekuwa namna moja muhimu ya kusambaza ujumbe kuhusu virusi na ukimwi **katika miji na vitongoji**.⁷¹

• 20% (114) ya vituo **vya kutoa ushauri na upimaji (VCT)** ipo mjini Nairobi, ilhalii huduma hizi hazipo katika **wilaya za mashambani**. Katika sehemu kama **Suba** ambapo kiwango cha ueneaji ukimwi ni 43%, kuna vituo 5 pekee vya kutoa **ushauri na upimaji (VCT)**, vingi vyake vikiwa **haviwezi kufikika na wanawake wengi**.⁷²

DONDODA NA MASUALA:

- "Suala la **kufanya mapenzi ni mwiko** katika jamii nydingi na itakuwa vigumu kwa wazazi kuelewa sababu za kijana kwenda kwa huduma za ushauri na upimaji (VCT)." (Mazungumzo na Kundi – lengwa la wanawake wachanga na wasichana, mashambani, umri 15–26)
